

# MPANGO WA KUJIFUNZA KWA MKUFUNZI (TUTOR LEARNING INITIATIVE): HABARI KWA WAZAZI, WATUNZAJI NA FAMILIA

Habari hii ni kwa wazazi, watunzaji na walezi juu ya Mpango wa Kujifunza kwa Mkufunzi (Tutor Learning Initiative), ambao utasaidia wanafunzi na kujifunza kwao katika 2021.

Mwaka wa shule ya 2020 umekuwa mwaka wa ajabu na changamoto kwa kila jamii ya shule.

Wanafunzi wengi wa Victoria walitumia muda mwingi wa Vipindi vya 2 na 3 mwaka huu kujifunza kwa mbali na shule za Victoria na jamii zao zimejitahidi sana kutoa mwendelezo wa ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wetu mnamo muda huu.

Mnamo Kipindi cha 4, shule kote Victoria zilikuwa zimeleenga kusaidia afya ya kiakili na ustawi wa wanafunzi, zaidi ya hayo kuwasaidia wanafunzi kuzoea tena kwa ujifunzaji wa mahali pa shule. Walimu pia wamelenga kutathmini ujifunzaji wa wanafunzi, kushughulikia mapungufu ya kujifunza na kuwatambua wanafunza wale wanaohitaji msaada ziada kwa ujifunzaji wao, kwa kutumia uchunguzi na tathmini katika darasa.

Tunajua kwamba uzoefu wa kujifunza kwa mbali ulikuwa tofauti kwa kila mwanafunzi. Wakati wanafunzi wengine walistawi, wanafunzi wengine hawakushiriki kikamilifu na ujifunzaji wa mbali. Kwa wanafunzi wetu wengi, ualimu wa kawaida wa hali ya juu mnamo 2021 utatosha kuwasaidia kuendelea hadi kiwango kinachotarajiwa cha ujifunzaji. Wanafunzi wengine watafaidika na msaada wa ziada wa kujifunza mnamo 2021.

Kama unayoweza kujua, kwa kujibu hili, Serikali ya Victoria inawekeza \$250 milioni katika Mpango wa Kujifunza kwa Mkufunzi (Tutor Learning Initiative) ili kuwezesha shule kote Victoria kutuma karibu walimu 4,100 kama wakufunzi katika 2021 kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji msaada ziada na kujifunza kwao. Shule zitaamua jinsi mpango huu utakavyotekeleza vizuri zaidi kwa wanafunzi wao na utahakikisha kuwa wanafunzi watapata msaada huu kwa njia inayopunguza usumbufu kwa shughuli zingine za ujifunzaji au za shule.

Kwa kutuma walimu wa ziada kusaidia watoto na ujifunzaji wa kina, walimu wa darasani watakuwa na uwezo mkubwa wa kuhakikisha kuwa mafanikio, ushiriki na mahitaji ya ustawi ya wanafunzi wote wengine yatatimizwa, ili wanafunzi wote wapate msaada wanaohitaji katika 2021.

Habari zaidi juu ya Mpango wa Kujifunza kwa Mkufunzi (Tutor Learning Initiative), na jinsi utakavyotekelezwa kwa wanafunzi wanaohitaji msaada wa ujifunzaji wa kibinafsi katika shule yetu, itatolewa kabla ya wanafunzi waanze kufundishwa mnamo 2021.

Mnamo Kipindi cha 4, shule zitashughulikia na wanafunzi kuelewa uzoefu wao wa kujifunza kwa mbali na wa kurudi kwa mahali pa shule.

Ikiwa una wasiwasi juu ya ushiriki wa mtoto wako katika ujifunzaji wao, wakati walijifunza nyumbani au baada ya kurudi kwa shuleni tafadhali wasiliana na shule yako.